# Jarida la UQAB

**Toleo 3**
**Aprili 2017 MILADI**
**Rajab 1438 AH**

**Kuupiga Vita Uislamu Kimfumo**

**Mujtama'a na Madawa ya Kulevya**

**Mchango wa Wanawake Katika Da'wa**

**Siasa za Vyama Vingi**




## Miaka 93 ya Kiza Kinene Kinachosubiri Mwangaza Wa Khilafah

# Miaka 93 ya Kiza Kinene Kinachosubiri Mwangaza Wa Khilafah



Tarehe 3 Machi,1924 sawa na 28 Rajab 1342 Hijiria, Dola ya Kiislamu (Khilafah) ilivunjwa huko Istanbul, Uturuki. Tukio hili lilitimiza ndoto mbovu ya wakoloni wakimagharibi ya kuiangusha Khilafah. Kwa kuiangusha serikali hii mkoloni Mwingereza Dola Kuu (Super Power) zama hizo alitaka Waislamu wasibakie tena na umoja wao waliokuwa nao kwa karne kumi na tatu. Umoja uliokuwa imara tena chini ya kiongozi (Khalifah) akitabikisha sheria ya Muumba wao Allah (swt). Haya hapa maneno ya aliyekuwa waziri mkuu wa Uingereza akasimulia tendo lao ovu la kuiangusha Khilafah: 'We must put an end to anything which brings about any Islamic unity between the sons of the Muslims. The situation now is that Turkey is dead and will never rise again, because we have destroyed its moral strength, the Caliphate and Islam". (Lazima tumalize kabisa chochote kile kiletacho umoja wa Kiislamu miongoni mwa Waislamu. Hali halisi sasa ni kuwa Uturuki imekwisha kufa na kattu haitorudi kusimama tena kwa sababu tumevunja nguvu/nishati yake ya kiimaadili nayo ni Khilafah na Uislamu.'

Baada ya kutumia vita dhidi ya Dola ya Kiislamu kama ilivyodhihirika tokea Mtume (saw) kuanzisha Dola yake Madina, makafiri walizua kila mbinu katika kuhakikisha kuwa Uislamu unabakia pasina na serikali. Licha ya Waislamu kuwa imara kwenye itikadi yao jambo lililowafanya wawashinde maadui zao lakini Wakoloni hawakukata tamaa ya kuvunja Khilafah. Wakaanza kuishambulia itikadi ya Kiislamu ambayo ndio uti wa mgongo wa Uislamu na nishati kubwa ya Waislamu katika kuwapa uhai na dira yao maishani. Wakapenyeza fikra za kizalendo, kitaifa, kikabila ndani ya Waislamu. Wakaja na njama nyengine nayo ni kuuchafua Uislamu na fikra zake hasa pale Waislamu wenyewe wakaanza kuitenganisha lugha ya Kiarabu ambayo ndiyo lugha iliyoteremshiwa kwayo Sheria za Kiislamu. Hali hii ikawafanya Waislamu wanakosa ufahamu safi wa Uislamu hivyo kupelekea kukumbatia hadhara ya Kimagharibi matata. Hapo ndipo Waislamu wakaanza kulemaa kiitikadi na kuwa rahisi Wakoloni kupata vibaraka ndani ya Umma wa Kiislamu kama vile Mustafa Kamal Ata Turkiy aliyefaulisha uovu wa kuvunjwa Dola ya Mwisho ya Kiislamu 1924!

Maana ya kuvunjika kwa Dola hii ni Waislamu kutohukumu na sheria za MwenyeziMungu (swt) badali yake wahukumiwe na kanuni za kitwaghut. Waislamu wagawanyike katika serikali za kikatuni zilizozochorwa na Wamagharibi na kupachikwa juu yake viongozi makhaini ambao ni wafu wanaojihesabu kuwa wako hai! Utajiri ulioko katika biladi za Kiislamu ukawa unaporwa na wamagharibi kwa niaba ya vibaraka hao. Umma ukabakia hauna hadhara ila hadhara ya kimagharibi wala hauna siasa ila ya kimagharibi. Naam, hivi ndivyo Umma ulipofikishwa. Kutia msumari moto damu tukufu za Waislamu zimegeuzwa kuwa damu za kunguni zinazomwagwa pasina huruma. Vilio, majonzi katika miji ya Kiislamu kuanzia Burma, Iraq, Afghanistan, Somalia, Yemen, Syria, Palestine n.k. Miaka 93 Umma hauna kiongozi! Umma umekuwa ukidhilalika mbele ya maadui wa MwenyeziMungu (swt) na Mtume wake na Waumini. Je tuendelee kunukuu na kushuhudia maafa juu ya maafa? Je hatujaona jinsi mfumo wa kirasilimali unakurubia kutangaziwa mazishi yake kwani ulifariki kitambo? Jamii ya Kiislamu inapaswa kutambua ufaradhi wa Kuisimamisha Khilafah. Naam, Khilafah sio ndoto wala mawazo ya kuwaza bali ni faradhi kwa Mola wetu ambayo kwayo nguvu na utukufu hupatikana. Ambayo kwa Waislamu hupata hifadhi. Kwayo Waislamu huweza kuhukumu na sheria za Muumba wao.

Wamagharibi waliangusha Khilafah na sasa Umma umezaa wanaume wanaoitaja Khilafah na kuilingania kwa hali na mali. Leo Umma kote duniani unaanza kuitamka na kuitaka. Dalili ya haya ni kuwa Wamagharibi wameanza kuichafua Khilafah kabla ya kusimama kwake. Vinatoka vipote vinavyodai Khilafah na kuangaziwa dunia nzima ilhali wanachofanya ni kinyume na Khilafah. Kwa upande wa pili wanaolingania Khilafah ya kikweli kwa usafi wake tena pasina na kubeba silaha hawaangaziwi na ikizidi wanapachikwa majina yakutamausha ikiwemo eti ni Magaidi au Watu wenye Msimamo Mikali! Twasema Khilafah ni

***Endelea Uk..3***



Email: uqab@hizb.or.ke

dola iliyoleta amani na utulivu kwa Waislamu na wasokuwa Waislamu leo yapakwa matope kuonyeshwa kuwa ni adui wa amani na usalama. Khilafah iliotingisha maadui mtingishiko mkubwa. Lakustajaabisha leo wanayoidai hawajatupa hata kombora moja kuinusuru Palestina dhidi ya mayahudi.
Naam, Waliivunja lakini Khilafah inakuja kwa mwendo wa kasi usiozuilika tena. Khilafah itakayo regesha tena haiba na kuhifadhi hadhi, heshima, mali na matukufu ya Waislamu popote walipo ulimwenguni kwa kuwanusuru dhidi ya kila fedheha na idhilali wanayofanyiwa. Khilafah inakuja kung'oa mfumo batili wa kibepari unaoangamiza vizazi na mimea. Khilafah inakuja kuwawezesha Waislamu kuhukumu na sheria za MwenyeziMungu (swt) na hapo ndio Allah atafungua Baraka zake mbinguni na ardhini. Lakini kuja huku kunahitaji wanaume wa kweli waliomuahidi MwenyeziMungu (swt), wanaume wasioshughulishwa na mauzo wala biashara ila kuilingania faradhi hii iliosahaulishwa kimakusudi. Wanailingania kwa njia ya Mtume (saw) aliyoichukua hadi kufaulu kuisimamisha Serikali ya kwanza ya Kiislamu katika mji wa Madina na hapo ndio waja wa MwenyeziMungu (swt) wakaishi katika nuru na kuingia katika Uislamu makundi kwa makundi. Tunaamini kiza hiki totoro cha udhalimu wa mfumo wa Urasilimali na nidhamu zake chafu ikiwemo ya utawala Demokrasia utaondoshwa na Khilafah itakayowakomboa walimwengu kutoka katika utumwa wa kuabudu wanadamu wenzao hadi kumuabudu MwenyeziMungu Muumba wa wanadamu.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**




**Habari**
Gavana wa Mombasa Hassan Ali Joho alifanya ziara hivi karibuni huko Marekani kuhudhuria mkutano wa kiulimwengu wa kupambana kile kiitwacho misimamo mikali. Ziara hii inakuja mwaka mmoja baada ya Mombasa kujumuishwa kwenye muuungano huo wa Mpango wa Miji Yenye Nguvu (Strong Cities Network (SCN)) uliofanya mkutano wake wa kwanza ulioleta pamoja mameya na magavana wa miji 25 kote duniani mnamo tarehe 30 Septemba 2015 huko New York.
**Maoni:**
Kulingana ripoti ya muungano huu wa (SCN) ni kwamba mpango huu ulianzishwa kitambo lakini ulizinduliwa rasmi Umoja wa Mataifa mwezi wa Septemba 2015. Mpango huu huwashirikisha wafanyibiashara, mameya, magavana pamoja na wawakilishi wa ngazi za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kubadilishana fikra na ujuzi katika kukabiliana na suala la misimamo mikali. Akihutubia waliohudhiria huko New York gavana Joho alionekana mkakamavu mno kuelezea malengo ya kongamano nayo ni haja ya kuwa na ruwaza ya kimikakati ya muda mrefu na kufanya mipango madhubuti ya kupambana na misimamo mikali. Joho alitangaza kubuniwa kwa kitengo cha kupambana na misimamo mikali kwenye ofisi yake ya ugavana. Akasisitiza haja ya kuwepo na ushirikiano na makundi ya kijamii hasa makundi ya kidini.
Ni wazi kuwa kongamano hili ni mfululizo wa ile kampeni ya kiulimwengu ya kupambana na Uislamu chini ya vazi la 'ugaidi na misimamo mikali'. Mikakati ya Marekani kwa sasa ni kushirikisha moja kwa moja Waislamu 'poa' waliofitinika na mfumo wake kusaidia kuupiga vita Uislamu. Ikumbukwe kua aliyekuwa raisi wa Marekani Barack Obama akihutubia vijana wa chuo kikuu cha Azhar Misri, mwaka 2009, alitaja kuwa Uislamu una chapa mbili:
Kwanza ni Uislamu usioafikiana na maadili ya kibinadamu na kimataifa huu ni ule ambao dunia nzima unapaswa kuupiga vita.
Pili ni Uislamu unaokwenda sambamba na maadili ya Kidemokrasia na fikra zake za utu na ubinadamu huu ndio Uislamu ambao pia Marekani inauunga mkono.
Ni jambo lijulikanalo kwamba Uislamu unapinga fujo za aina yoyote ile na pia njia yake ya kuutekeleza katika nyanja za maisha sio ya kutumia mabavu, lakini juu ya hayo Wamagharibi hawatokoma kuushambulia Uislamu na kujaribu kuubadilisha. Uislamu umeeleza bayana kuwa Mwenyezi Mungu pekee ndiye Aliye na haki ya kutueleza kuwa matendo haya ni mazuri au ni mabaya. Mtume (saw) amesema katika hadithi: Mwenyezi Mungu amefaradhisha faradhi (Matendo ya wajibu) hivyo msipoteze faradhi hizo. Na akaharamisha mambo wala msiingie ndani yake na akaweka mipaka wala

*Endelea Uk..4*

msiivuke na akanyamazia baadhi ya mambo ile ni rehema kwenu nyinyi wala sio kuwa yamesahauliwa. Msimamo mzuri ni ule anaouridhia Mwenyezi Mungu na mbaya ni anaouchukia. Na yoyote anayekiuka mipaka ya Uislamu huyu amevuka mipaka. Lengo hasa la Marekani kuleta misamiati hii ni kutaka Waislamu wautupilie mbali Uislamu wao. Ilhali Wamagharibi ambao huku wakisisitiza kuwa vita dhidi ya ugaidi sio vita dhidi ya Uislamu, hao hao ndio wanaoshambulia sheria za Uislamu kama vile Jihad, Khilafah n.k. Tayari vijana wa Kiislamu katika baadhi ya mataifa ya kimagharibi kama vile Uingereza, wanaojiepusha na unywaji pombe huitwa wenye misimamo mikali.

Kwa hivyo kupachikwa Waislamu au makundi ya Kiislamu majina ya siasa kali, misimamo mikali au magaidi ni kisingizio tu cha kuwasukuma Waislamu ulimwenguni waachane na Uislamu wao kama mfumo wa haki ili waendelee kujifunga na mfumo muovu wa Urasilimali. Ni jambo la kuvunja moyo sana kuona wanavyuoni wa Kiislamu wamekubali kuburutwa na kuingizwa kwenye mtego wa vita vya wamagharibi vya kuupiga vita Uislamu na fikra zake.

Misemo hii ya siasa kali, mafundisho yenye itikadi kali na kadhalika haikuwa ila jaribio la Amerika kuubadilisha Uislamu aliyokuja nao Mtume (saw) kama suluhisho kwa matatizo ya wanadamu wote.

Kwa bahati mbaya, Waislamu wameshindwa kuelewa uhalisia huu na sasa wanatupiana lawama na kujigawa katika misingi aliyoitaka Marekani. Leo wako Waislamu wanaombiwa itikadi kali, siasa kali na wale Waislamu wanaoitwa wenye misimamo ya kadri au poa. Misamiati hii hukaririwa na vyombo vya habari ambavyo ni zana za kueneza propaganda za kimagharibi dhidi ya Uislamu na Waislamu. Tayari Waislamu wenyewe wanaonekana wakijigawa kimakundi na kupelekea kupigana vita wao kwa wao kwa sura ya Vita vya wenye misimamo mikali dhidi ya Wenye misimamo poa'. Lakini ukweli ni kwamba imani kali, misimamo mikali na ugaidi yote hii ni misamiati iliyochovywa siasa ndani yake inayotumiwa kuushambulia Uislamu kifikra baada ya kushambuliwa tayari kijeshi ambapo walishindwa.

Wamagharibi pamoja na vibaraka wake wamefaulu katika kuwasukuma Wanasiasa na wanavyuoni wa Kiislamu kucheza mchezo hatari wa kukubali kuwa ati Waislamu ndio tishio la usalama duniani. Waislamu tayari wameingia kwenye mtego wa kuutangazia vita Uislamu chini ya madai ya kupambana na Ugaidi, imani kali na misimamo mikali.

Hata ikiwa kweli zipo tofauti baina ya Waislamu lakini hazifai kutumiwa tofauti hizi kama sababu ya kutaka suluhisho kutoka serikali za Kisekula zinazoendeleza unyanyasaji na udhalilishaji wa Waislamu na Uislamu. Kinachotakikana ni kuwa tofauti hizi zenyewe ziwe sababu ya kuchangamka Waislamu wafanye bidii ya kuleta mabadiliko ya kweli kwa kusimamisha Khilafah itakayoongozwa na Amiri mmoja aliye na mamlaka ya kutatua mizozo baina ya Waislamu na kuhifadhi hadhi, heshima, mali, matukufu yao na kusambaza amani na ustawi ulimwenguni kote.

وَلَن يَجْعَلَ ٱللَّهُ لِلْكَـٰفِرِينَ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا

"Wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini"
[An-Nisaa: 141]

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**



# Mujtama'a na Madawa ya Kulevya

Hakika utumiaji wa mihadarati na pombe ni jaribio la kiwango cha muamko ama kuporomoka kwa mujtama'a. Utumiaji wake ni jangaa kuu kwa njia zote na huregesha nyuma jamii, huvunja mahusiano na maingiliano yote ya kijamii. Hubadilisha miji kuwa pori na wanadamu kudunika kushinda wanyama. Maadili mema kutokana na kujidhibiti mpaka subira, ukweli mpaka uaminifu yote yamepotea kwa sura ya jamii. Ikiweka nidhamu zote za mujtamaa kuanziya ya utawala, kisisasa, mahakama, usalama, uchumi na kadhalika katika hali tata. Insha'Allah tutaangalia chanzo cha athari za mihadarati na kiwango gani mihadarati na pombe zimefisidi nidhamu yote. Wanadamu wako na mahitaji ya kiviungo na mahitaji ya kihisia, kushibisha yote hulazimisha nidhamu ambayo itakayoongoza, kupanga na kuekea ratiba njia zote za kushibisha, nidhamu ambayo inawiyana na umbile la mwanadamu na sio ile inagongana nalo. Utu wa binadamu ni akili na nafsiya(kitabiya), kupima matendo na vitu vinavyo mskuma mwanadamu kufikia kutimiza hisia

*Endelea Uk..5*

zake kupitia fikra maalum(itikadi). Hivyo basi kurudi nyuma kwa mwamko ni matunda ya fikra maalum (nayo ni itikadi) inayo muongoza mwanadamu katika kushibisha mahitaji yake ya kiviungo na kihisia.

Hali iliyo sasa, kiulimwengu itikadi inayo tawala ni fikra za kidunia (secular) ambayo imetokana na nidhamu inayotabikishwa kama suluhisho la mas'ala jumla ya maisha. Fikra za kidunia (secular) zimekuja kama mazao ya suluhisho la kati na kati baada mapenduzi ya europa. Mapenduzi yaliopatikana kupitia umwagaji wa damu yaliozaa fikra maalum kuhusu dini, maisha na siasa; kumvua ubwana muumba wa mwanadamu, maisha na ulimwengu na kumpa mwanadamu cheo hicho.

Ubwana katika itikadi ya kidunia (secular) nikuwa mwanadamu ako na uweza wakujitungia sheria na kujiamualia zuri na baya kinyume na mafundisho ya mola. Hizi ni fafanuzi/ taarifa za kimakosa zinazotokamana na fikra za wanadamu ambazo zinatofautiana kiuweza wa kiakili ambayo ni kinyume na hugongana na asili ya mwanadamu. Kwa mfano furaha ni nini? furaha kama hisia za mwanadamu hazina ufafanuzi wa wazi, lakini katika itikadi ya kidunia(secular) kutafta furaha kumewafanya watu kujitosa kwa kila aina ya vitendo kufikia kilele cha raha. Misemo kama "kua tajiri ama kufa ukijaribu (get rich or dying trying)" ama "fanya tu (just to it)" yamekua kama kumbukumbu ya matendo yakufikia furaha.

Fikra za uhuru zimetengeza jamii isiowajibika na kucha hufanya juhudi yakutafta raha ambayo niyakidanganyifu badili yakweli. Kuamini kuwa kujiridhisha kimwili na kumiliki vitu ndio funguo za kupata kilele cha furaha; athari zake ni mkazo wa kihisia (stress) wa hali ya juu, huzuni na uchovu na zimwekua ni sononeko la kiulimwengu likizalisha kukata tamaa na fikra ya kukwepa kutoka hali halisi iliyo na dhiki kwa kutafuta vishuhuli na afuweni kutokamana na ukweli usio ridhisha kupelekea watu kwa jamii kujitosa kwenye mihadarati na ulevi.

Hii ni katika upande wa mzizi wa haya kuwa ni itikadi ya kidunia(secular), lakini kuna sababu nyengine ikiwemo uraslimali kama mfumo wa uchumi wa itikadi ya kidunia(secular), mfumo uliokusanya utajiri kwa mikono ya wachache. Majuzi shirika la OXFAM lilitoa ripoti ya watu wanane wenye umiliki wa utajiri wa hali ya juu kushinda zaidi ya nusu ya idadi ya watu ulimwenguni (bilioni 3.6) ikizaa hali kukata tamaa ya kiuchumi. Kudhibiti mali kwa mikono ya wachache nikukanusha nadharia ya fikra ya "kuwa wenye mali ama mashirika makubwa yakinufaika basi jamii yote hunufaika (trickledown theory)" kuwa ni fikra isiowezekana na yakiuongo. Vipimo vya matendo katika itikadi ya kidunia(secular) ni maslahi na faida, na kwakua mihadarati kama "bidhaa ya kiuchumi" huleta faida kubwa kupitia ulanguzi wa madawa ya kulevya. Magenge ya wauzaji mihadarati wakishirikiana na wafanyikazi wa serikali nao ni wausalama, wanasheria na mpaka wakuu watendaji wa nchi kushirikiana na kuunda vikundi vya mashirikiano katika kueneza mihadarati. siajabu imechkua amerika zaidi ya miaka 100 mpaka leo kupigana vita juu ya walanguzi wa madawa ya kulevya bila ishara yoyote ya kushinda vita hivi bali uongezeko wa uzalishaji na mahitaji yake kufanya ulanguzi wa madawa kuna ndio sekta inayo ongoza ya kuchumi miongoni mwa sekta nne zina zo ongoza ikiwemo mafuta, silaha na sekta ya urembo. Katika chum wa kiraslimali, mihadarati na pombe huchkuliwa kama sehemu asili ya nidhamu ya kimaisha. Uchafu wa mihadarati kihakika ni matunda ya uraslimali.

Nidhamu ya kijamii katika itikadi ya kidunia(secular) imefeli pakubwa katika kufafanua majukumu msingi ya mwanamume na mwanamke katika maisha ya ndoa na mjumuiko wa kijamii ambapo kumejenga pengo kubwa katika malezi na majukumu ya kijamii. Badili yakua na kizazi kinachoenda sambamba na kizazi vya nyuma bali tunavyo vizazi vyakuzorota, viumbe vigeni badili yakua ni vizazi. Heshima, maadili na kujali imetoka katika malezi. Malezi yakawa ni kulisha, kuvisha, kupeleka watoto shule bila malezi ya wazazi ambayo yako mbali na kulea kizazi cha kuwajibika.

Itikadi ya kidunia (secular) inafafanua jamii kama mkusanyiko wa watu wenye fikra, rai na maslahi tofauti, na unakuza uwingi na ubinafsi kiasi yakua makundi na watu wenye maslahi tofauti kuamini wamedhaminiwa kama makundi ya mashoga, vyama vya kisiasa, na dini lakini ikiambatana na msingi wa kidunia(secular) wala sio kugongana. Fafanuzi hii ya kimakosa imetengeze watu kwa misingi ya kiubinafsi na kimakundi kwenye jamii inayojali mas'ala ya kiubinafsi na kuacha jukumu la jumuia kwa serikali. Ndio Uislamu unachkua uchafu huu kama mama wa maovu yote kama vile mtume (saw) alivyosema "Tembo(vilevi) ni mama(mzizi) wa machafu". Ni wajibu wa mujtama'a wakiislamu jumla kuamrisha mema na kukataza maovu. allah (sw) asema:

وَلۡتَكُن مِّنكُمۡ أُمَّةٞ يَدۡعُونَ إِلَى ٱلۡخَيۡرِ وَيَأۡمُرُونَ
بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَوۡنَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِۚ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ

"Na uwe kutokana na nyinyi umma unao lingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio walio fanikiwa"

[Al-i'Imran: 104]

Jukumu ni la kijamii na kisiasa pale jamii itakapowahisabu wenye kufanya maovu haya na wakati huohuo kuhisabu uongozi wa serikali kutekeleza jukumu la kuondoa uovu huu kutoka kwa mizizi yake nayo ni uzalishaji. Sheira ya kiislam imeeka sharia kali kwa wanyekupatikana na hatia kwa Nyanja zote za muovu huu na kueka adhabu kali kwa wenye kueneza ufisadi, kuzalisha na kusambaza mihadarati na kueka mpaka adhabu ya viboko themanini kwa walevi wanaoleta machafuko hadharani.

**Ali Omar**

# Mchango wa Wanawake Katika Da'awah



كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ ۗ وَلَوْ ءَامَنَ أَهْلُ ٱلْكِتَٰبِ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُم ۚ مِّنْهُمُ ٱلْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ

"Nyinyi ni Ummah bora ulioletwa kwa watu,munaamrisha mema na kukataza maovu na munamuamini Allah,"[Al-Imraan -110].

Allah (SWT) anatusifu sisi kama umma wa Mtume Muhammad (SAAW) ndio umma bora kwa sifa yetu ya kukanyana maovu na kuamrishana mema. MwenyeziMungu SWT hajahusisha ubora huu mwanamke wala mwanamume bali ni kwa waislamu wote. Kwa maana haya mwanamke hakuachwa katika jukumu la kubeba da'awa ya kukataza maovu na kuamrisha mema.

Katika ulinganizi wake Mtume (saw) kuleta mageuzi, aliwahusisha wanawake kivitendo nao pia katika kadhia hiyo adhwimu ya kuulingania Uislamu. Ndio tunawaona wanawake walio na sifa zisizokuwa na mfano kama Khadija (ra) ambaye hakuwa tu mke wa Mtume (saw) bali mtu wa kwanza kuukubali Uislamu, mtu wa kwanza kuungana mkono wito wa Uislamu kwa kutoa mchango kwa Da'wah si tu kifedha bali na zaidi; na Sumeiya (ra) shahidi wa kwanza katika Uislamu aliyesimama kidete dhidi ya adhabu na mateso yasomithilika kutoka kwa makufar wa Makkah zama hizo za Da'wah. Hiyo ni baadhi mifano katika orodha ndefu ya wanawake jasiri katika historia ya Waislamu. Bila kusahau hali ilivyo leo na wakati huu ulimwenguni kote ni sawa na ilivyokuwa ndani ya Makkah takribani karne 14 zilizopita; ulimwengu unaongozwa na ukafiri wa mfumo wa urasilimali ambao umetanganisha Muumba wa mwanadamu na Serikali. Hali hii inatoa nafasi kwa wanawake kuandikwa katika vitabu vya khair vya Mwenyezi Mungu kwa kuhusika katika mchakato wa kuwakomboa wanadamu kutoka katika minyororo ya kuabudu vilivyoumbwa/warasilimali hadi kumuabudu Muumba wa mwanadamu, ulimwenguni na uhai. Wanawake wanaweza kuchangia katika kadhia hii adhwimu kwa kuulingania Uislamu Kimfumo ndani au kwa familia zao, watoto wao, kaka zao, dada zao na marafiki popote watakapokutana au kila nafasi inapojitokeza ya wao kutangamana.

Licha ya mwanamke kuwa na jukumu lake la kiasili nalo ni mlezi wa watoto bado anawajibika kama Muislamu kubeba daawa. Huku akistahiki kuwanyonyesha watoto wake pia ana wajibika awafundishe tarbia/malezi mazuri ili wakue kishakhsiya za Kiislamu hatimamye waweze katika mustaqbali wabebaji Uislamu. Wanawake wa kiswahaba (Allah awe radhi na) walifahamu majukumu yao kama Waislamu na ndio maana wakajitosa kwenye ulingo wa daawah na wakaweza kuinusuru kihali na mali.Wanawake hawa wema waliotangulia,walimlilia Mtume (SAAW) awatengee wakati wa kuwafundisha Uislamu ili waweze kujifunga nao. Waliwalilia ngoa wanaume pale walipokuwa wakionekana wakiwa msitari wa mbele zaidi kwa Mtume SAAW katika mas-ala ya kutafuta elimu. Naye Mtume SAAW pasina kuchelewa akawasikiza na akawatengea siku yao akawa anawafundisha na kuwaongoza katika masaala ya kiislamu.(Bukhari)Wanawake hawa walijitolea kusoma na kuujua uislamu wao na kuufanyia kazi.

Wanawake wa Kiislamu waliotutangulia waliwafunza wanawao Uislamu. Kwa mfano tu,Ummu Sulaim alimfundisha mwanawe Anas ibn Malik Uislamu,Nana Aishah (R.A)alikuwa mwalimu mzuri si kwa kwa swahabiyat pekeebali mpaka kwa maswahaba...lau tutawataja wanawake waliotekeleza jukumu hili la daawah basi hatutamaliza.

Wanawake wa Kiislamu wa sasa tumejisahau na majukumu kama haya,tumewaachia wanaume pekee jukumu la kuamrisha mema na kukataza maovu,ilhali sisi ndio tulio na mchango mkubwa katika hili,tuna nafasi nzuri na watoto wetu na pia na wanawake wenzetu,tunaweza kutekeleza jukumu hili barabarani,sokoni,harusini,mazishini na kokote kule tunakokutana kama wanawake.

Mtume (SAAW)asema,"atakae ona munkar basi na aukataze kwa ulimi wake,au kwa mkono wake na akishindwa basi achukie kwa moyo wake na hii ni miongoni mwa iman dhaif,"Imam muslim kutoka kwa Abu Said Khudri.Hadith hii haifwatwi siku hizi na wanawake ndio kabisa hatulitekelezi hili. Tunapokusanyika wanawake tunaona munkar umafanyika ila hatuukanyi,ndugu zet wanatembea uchi hatuwakanyi ila tunataka kuiga,riba zanaliwa hazizuiliwi,zina inatekelezwa haikanywi na kibaya zaidi kuchukia

*Endelea Uk..7*

ambayo ni imani dhaifu pia hatuchukii.
Matatizo yanayotukumba maishani kamwe hayatoisha lau hatutatekeleza jukumu hili.Ubebaji daawah si rahisi hivyo basi yataka kujitolea kwa mtu kama walivyojitolea waliotutangulia. Wanawake wema waliotangulia walilea watoto wakakuza mujahidiina,wakakuza maANSWAR na MUHAJIRINA.Wakakuza jeshi la kiislamu,leo kwa kuzembea wanawake katika hili,tunakuuza vijana wenye tabia na mienendo ya ajabu ajabu,ALLAH atuongoze ummati Muhammad!
Tumeghafilika na jukumu hili la kuamrisha mema na kukanya maovu,na kujiingiza kwenye siasa za kikafiri za Kidemokrasia tunakofikiri ndiko kuliko na mwangaza wa giza la matatizo liliotugubika.Lau kama twatekeleza alioyotuamrisha ALLAH (swt) basi hadhi ya mwanamke ingetambulika vile ilivyosahaulika leo. Wanawake wa kiislamu tuacheni kulilia nafasi kwenye siasa za kikafiri bali turudi kwenye siasa zetu alizotuekea Allah(swt),tuchangamkieni majukumu yetu ya kisiasa kiislamu kama walivyowajibika wanwake waliotutangulia,hakika sisi ni miongoni mwa umma bora...

**Mgeni Juma**

# Siasa za Vyama Vingi: Uongo wa Kidemorasia



Tangu kuregeshwa tena kwa Siasa za Vyama Vingi 1992, umoja wa upinzani umekuwa jambo linalohitajika lakini lisilowezekana hususan tunapolenga uchaguzi wa uraisi. Tofauti na 2002 ambapo vyama vya upinzani rasmi villiungana pamoja na kuiangusha KANU iliyokuwa imekalia uongozi kwa miaka mingi. Tatizo kubwa likiwa ni kutoelewana na kukosekana umoja ndani ya upinzani kila kukifikia uchaguzi. Matukio ndani ya miezi ya hivi karibuni yanaonyesha muamko wa ari hii lakini ikiwa imejivika katika sura za kibinafsi za wanasiasa wote. Februari 22, 2017; Muungano wa Kitaifa wa Upinzani (NASA) ikiongozwa na Raila Odinga, Kalonzo Musyoka, Moses Wetangula na Musalia Mudavadi walitia sahihi mkataba wa kugawanya mamlaka ambao utawawezesha kuungana katika uchaguzi wa Agosti 8. Katika mkataba huo ipo njia ya kugawanya viti vya juu lau watashinda. Miongoni kwa mapendekezo ni kuweko kwa nafasi ya Mkuu wa Mawaziri ambayo kwa mujibu wa wandani wa upinzani itamwendea mmoja wa wagombaniaji atakayeibuka wa tatu katika kinyang'anyiro cha uraisi wa kupendekeza. Makubaliano hayo yanasema kuwa lau watapata ushindi, raisi wa NASA atakuwa na nguvu za utekelezaji zitakazomuezesha kubuni Ofisi ya Mkuu wa Mawaziri. Kisha Muungano huo utaitisha mabadiliko ya kikatiba ili kubadilisha Ofisi ya Mkuu wa Waziri hadi Waziri Mkuu. Vyeo vingine ambavyo NASA inalenga kuvitumia kumakinisha muungano wao katika mamlaka ni pamoja na Spika wa Seneti, Mkuu wa Wengi Bungeni na Mkuu wa Wengi Seneti. Msingi wa mpango huo ni kuhakikisha kuwa vigogo wanne wa NASA wanapata nafasi katika serikali lau muungano huo utaibuka mshindi katika uchaguzi wa Agosti 8.

Licha ya kuwa wanaoneka kudhihirisha umoja, matukio ya hivi karibuni yameashiria kuwa mambo hayapo sawa ndani ya muungano wa upinzani. Januari 13, 2017; gazeti la The Standard liliripoti kuwa muungano huo wa umoja wa Upinzani uko njia panda katika jina jipya – Muungano Mkubwa wa Kitaifa (NASA) au Muungano wa Mabadiliko na Demokrasia (CORD). Baadhi ya vigogo wa Upinzani walikuwa wanasita kujiunga chini ya mrengo wa NASA kwa kuwa kiongozi wa chama cha Muungano wa Kitaifa wa Amani (ANC) – Musalia Mudavadi ndiye aliyebuni wazo hilo na ulikuwa umesajiliwa na Katibu Mkuu wake. Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari Nairobi tarehe 12 Februari, 2017; Wetang'ula alisema kuwa viongozi wa Upinzani hawajawahi kuwa na mazungumzo kuhusu NASA kama muungano wao mpya wakielekea katika Uchaguzi wa Agosti 8. “Sisi ni CORD. Twahitaji kuamua nini tena? Nini kipo katika jina? Yeyote anayetaka kujiunga nasi ana karibishwa. Twamkaribisha Mudavadi kujiunga nasi,” alisema Wetang'ula. Sintofahamu kuhusu jina ilijitokeza tena pale Seneta wa Siaya James Orengo aliposoma tamko la pamoja lililotiwa sahihi a viongozi wote waliokuwepo Bomas, ambalo halikutaja NASA lakini walizungumzia kuhusu “jukwaa la pamoja la Upinzani”. Walio na mtizamo wa

*Endelea Uk..8*

uchambuzi waliweza kuona kuwa mkutano wa Bomas ulikuwa kama 'muungano' wa wasiotaka.

Ama kuhusu kura ya Luhya, pale Mudavadi alipotawazwa kuwa kiongozi wa waLuhya mjini Kakamega, mara tu viongozi wa FORD Kenya waliitisha kongamano la wanahabari na kumkana. Kutofurahishwa kwa FORD Kenya kuhusu kurudi kwa Mudavadi ndiyo chanzo cha kutoshikamana ndani ya Upinzani. Napia inachangia katika kukosekana umoja na kuwa tishio kwa ndoto ya kuelekea Ikulu. Kwani kati ya Mudavadi na Wetang'ula mtu mwenye kura ni Mudavadi. Katika kura zilizopita Mudavadi alipata kura zaidi ndani ya eneo hilo mara nne ya Wetang'ula ambaye alishindwa kupata kiti cha eneo bunge la Sirisia nyumbani kwake ambacho kilikwenda kwa ODM. Lakini nukta ya Bukusu ndani ya siasa za waLuhya lazima zieleweke. Yapo makabila 18 madogo ndani ya kiukoo na wanaunganishwa kwa lugha moja. Kisiasa, kila kunapochipuka kiongozi wa waBukusu kama "Kigogo" wa Luhya basi jamii yote humkubali na kumzunguka. Kinyume na kuwepo kigogo kutoka kabila jengine dogo, wa Bukusu hawampokei kwa moyo mkunjufu. Naye Wetang'ula akitoka katika Bukusu, nukta hii inaleta sintofahamu katika umoja wa upinzani. Lau Jubilee itapatiliza nukta hii ili kuwaweka Bukusu kutoka kwa waLuhya, hili bila shaka litawaudhi na kuwanyima upinzani kufikia madaraka. (https://www.standardmedia.co.ke/article/2000229755/bukusu-factor-hangs-above-new-found-opposition-unity)

Ama kumhusu Kalanzo, amejipata katika hali ngumu mwaka mmoja kabla ya kura zijazo. Anakumbana na upinzani ndani ya eneo lake la Ukambani ambapo mpinzani wake wa jadi, Charity Kaluki Ngilu, anayegombania kiti cha ugavana na inatarajiwa kuwa ataupinga uongozi wa Kalonzo Ukambani. Napia yupo Gavana wa Machakos, Alfred Mutua ambaye naye anazuru eneo hilo akiwa na lengo wazi la kung'oa chama cha bosi wake kama kiongozi asiyepingwa wa waKamba. Haya yanamuacha mtu mmoja kuwa na uungwaji mkono wa kabila lake na sura ya kitaifa amabye ni Raila. Ama anachagulika au la; hilo ni suala jengine tofauti. Hata hivyo, kuumakinisha umoja huu hatuna budi kukumbuka yaliyotokea 2007, azma za siasa za kibinafsi na ulafi yanatarajiwa kudhihirika ambapo mazungumzo ya siri ya usiku kuhusu madaraka yatajirudia mara nyingi kabla siku ya uchaguzi Agosti 8. Mikutano ya siri itafanyika ili kuzungumzia maslahi ili kupata vyeo katika serikali. Huu ndiyo ukweli kwa mujibu wa siasa zetu za kikabila ambazo daima zitajirudia kila inapofika wakati wa uchaguzi.

Ama kuhusu Serikali ya Jubilee, iliripotiwa na gazeti la Standard, Februari 26, 2017 ya kwamba viongozi wa kuu wa Chama cha Jubilee (JP) wanakubali kuwa uvunjaji wa vyama vidogo ulikuwa si maamuzi mazuri na hayakufanyika wakati mzuri. Hili linatokea wakati watu wanahamia katika vyama vidogo ambavyo vinazidi umaarufu katika sehemu za Jubilee; ikilifanya wazo la kuunda cha kimoja chenye nguvu kuwa wazo lisilomaana. Hivi sasa wanasema ndoto kubwa ya kutengeneza chama kimoja kikubwa JP ambacho kingeliweza kumeza vyama vidogo ndani ya maeneo ya Mlima Kenya na Bonde la Ufa; imefeli. Seneta wa Meru, Kiraitu Murungi ambaye alikuwa mwenyekiti wa kamati endeshaji ambayo ilisimamia hatua ya kuunganisha vyama akiwa pamoja na waziri wa zamani Noah Wekesa, walisema kuwa kuunganishwa vyama vya kisiasa kuwa JP lilikuwa wazo zuri la kinadharia lakini kiutendaji wake umefeli. Kamau Wairuri, mchanganuzi wa kisiasa anaashiria baada ya muda ndani ya miezi ijayo JP itang'amua kuwa hatua yote hiyo haitozalisha waliyotarajia. "Watafikia hitimisho kuwa kuanganisha vyama vya kisiasa labda ulikuwa mpango mzuri lakini haudhamini mafanikio. Uunganishaji huo ulilazimishwa kwa vyama ndani ya Muungano huo, ilhali huku kwa pigwa vita mganwanyiko na sauti za kumakinisha. Mzozo utakaochipuka katika kura ya kupendekeza inayotarajiwa kufanyika katika JP itapelekea serikali iliyoko mamlakani kutokuwa sawa kabla tarehe ya uchaguzi. Vita baina ya walioko mamlakani na wanaogombania viti tofauti vya uchaguzi, haswa vya Ugavana na Uwakilishi wa Wadi katika maeneo yenye nguvu ya chama; yatakuwa makali na mizozo itakayochipuka haitosawazika!

Siku ya Jumapili Februari 26, 2017, gazeti la Nation liliripoti kuwa timu ya kuhakikisha Raisi Uhuru Kenyatta anachaguliwa tena imeandaa mikakati kabambe ili kupata ushindi katika uchaguzi wa Agosti 8, ikiwemo pamoja na mapendekezo ya kubuni vyeo vya Manaibu wa Raisi viwili na kimoja cha Waziri Mkuu. Ili kufikia mabadiliko hayo yanayohitajika kikatiba; maandishi hayo ya siri yanapendekeza kuwa uongozi wa Jubilee uwape mkono upinzani na kuwarai wakubali mabadiliko yaliyopendekezwa ili kuibaidili sura ya serikali. "Serikali yaweza kuwahusisha na kukubaliana na CORD kuhusu uwezekano wa kubadilisha Katiba ili kuongeza mapendekezo hayo katika ngazi ya Uraisi" yanasema. Ifahamike kuwa CORD ambayo sasa imegeuka na kuwa NASA inashikilia mawazo hayo pia. Tukielekea katika msimu wa uchaguzi, maandishi hayo yanatoa orodha ya masuala ambayo timu ya UhuRuto ya tena wajitayarishe nayo hata katika maeneo yao yenye nguvu ni kutotimiza ahadi walizotoa, kutowapa baadhi ya jamii nafasi serikalini, utovu wa usalama, siasa za mshika hatamu 2022, ufisadi na mengineyo.

Kuhusu zoezi la usajili wa kura, lilidhirisha wazi kuwa zoezi hilo limeiweka nchi katika hali ya uchaguzi mapema. Idadi ya mapema iliyotolewa na Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) imeonyesha kuwa jumla ya 3.7 milioni ya wapiga kura wapya wamejisajili ndani ya zoezi lililoisha hivi karibuni. Huku maeneo yenye nguvu JP na NASA yakirekodi

*Endelea Uk..9*

idadi kubwa ya waliojitokeza. Idadi inaonyesha kuwa kitabu cha kusajili wa wapiga kura imeongezeka hadi 19,562,690 ya wapigaji kura licha ya kwamba Tume bado itafanya zoezi zito lakuisafisha rejista ili kuwaondosha waliokufa na walio chini ya umri ya upigaji kura na wangineo wasiostahili. Wafula Chebukati, Mwenyekiti wa IEBC alipokuwa anatoa matokeo ya zoezi la usajili wa kura alikadiria zaidi ya majina 0.5milion yatatolewa! Ama takwimu zilizotolewa na IEBC zilionyesha kuwa kunatarajiwa mashindano makubwa kinyume na hapo awali ikitarajiwa kuwa maeneo yenye nguvu ya NASA yataweza kujipatia7.3milioni ya wapigaji kura tukilinganisha na maeneo yenye nguvu ya Jubilee kutoa 7milioni ya wapigaji kura. Huku mirengo yote ya kisiasa ikipigia jicho ushindi ilhali watafiti wanaonya kuwa kinyang'anyiro cha 2017 kitashindwa na chama kitakachoweza kuhakikisha kinatoa wingi wa wapigaji kura kuliko wa pinzani wao. Kando na usajili kuna shaka ya uhakika kuhusu IEBC kuytojiandaa vyema kuhusu uchaguzi wa Agosti. Idadi kubwa yam ashine za BVR zimeripotiwa kuwa hazifanyi kazi ilhali upeperushaji wa matokeo ya uraisi bado yamekwama katika mzozo wa njia itakayotumiwa.

Sasa imekuwa mtindo kwamba kila msimu wa uchaguzi nchini Kenya kunabuniwa 'muungano mkubwa' mpya na ahadi mpya za mabadiliko. Majina yanayonasibishwa na miungano hiyo bado yanabakia kuwa yale yale na yenye uungwaji mkono kikabila na ahadi wanazoahidi miungano hiyo kwa njia ya kura hazibadiliki. Kwa wasomi wa kisiasa Kenya, raia ni bidhaa inayogawanywa katika misingi ya kikabila na kupigiwa debe na kuuzwa! Tunatoa mwito kwa Umma wa Kiislamu kuwa uwe macho na mipango miovu ya siasa za kikafiri ambazo zinachezwa na kuoneshwa kama suluhisho la mwanadamu. Hakuna manufaa yanayopatikana kutoka kwenye nidhamu ambayo watu wake ni walafi na wasiojali maendeleo ya Umma. Ni umoja wa Waislamu chini ya kivuli cha Serikali ya Kiislamu ya Khilafah amabyo itatuondoa sisi kutoka katika nidhamu hii inayonuka na iliyofeli ya Demokrasia. Na tukielekea katika Uchaguzi Mkuu tukumbuke ya kwamba Mwenyezi Mungu amebainisha wazi kwamba:

إِنِ ٱلْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ ۚ أَمَرَ أَلَّا تَعْبُدُوٓا۟ إِلَّآ إِيَّاهُ ۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

"Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka. Lakini watu wengi hawajui"

[Yusuf: 40]

**Kassim Agessa**

# Kampeni ya #3Machi1924













